

13G-At-Ta'aanuq (Kisimamo Cha Kujumuika Pamoja)

التَّعَانُق At-Ta'aanuq

Hiki ni aina nyingine ya kisimamo nacho ni visimamo viwili kwa pamoja ambavyo huweko pamoja katika Aayah moja baina ya neno na neno au baina ya kauli na kauli ya Allaah (سبحانه وتعالى) na msomaji huruhusiwa achague kimoja asimame, kwani kisimamo ni kimoja tu; hivyo akichagua kusimama katika alama ya mwanzo basi ya pili yake atatakiwa asisimame bali aendelee kusoma; na ikiwa atachagua kutosimama katika alama ya mwanzo basi atatakiwa asimame katika alama ya pili yake.

Alama kisimamo hichi ni vidoti vitatu kama hivi ❖ ❖ ❖

- Mfano wa kwanza:

الْم ﴿١﴾ ذَٰلِكَ الْكِتَابُ لَا رَيْبَ ۚ فِيهِ ۚ هُدًى لِّلْمُتَّقِينَ ﴿٢﴾ ¹

((Alif Laam Miym)) ((Hiki ni Kitabu kisicho na shaka, ndani yake ni Hidaayah kwa wenye taqwa))

Bonyeza usikilize

Inafaa kusimama katika:

لَا رَيْبَ ۚ

kwa sababu imekamilisha maana yake kwamba: ((Hiki ni Kitabu kisicho na shaka)). Kisha kuanza na:

فِيهِ ۚ هُدًى لِّلْمُتَّقِينَ ﴿٢﴾

kwa sababu pia inaleta maana iliyokamilika kwamba ((ndani yake [Hiki Kitabu] ni Hidaayah kwa wenye taqwa)).

Au badala yake kusimama katika:

¹ Al-Baqarah (2: 1-2)

فيه

kwa maana: ((Hiki ni Kitabu kisicho na shaka, ndani yake))
kisha ukamalizia kusoma:

هُدًى لِّلْمُتَّقِينَ ﴿٢١﴾

((Ni Hidaaya kwa wenye taqwa))

Lakini haipasi kabisa kusimama katika alama zote mbili kwa sababu itaharibu kabisa maana.

- Mfano wa pili:

Inapasa kusimamia neno **وَتَمُودَ** au kusimamia neno **بَعْدِهِمْ** katika kauli ya Allaah:

أَلَمْ يَأْتِكُمْ نَبُؤُا الَّذِينَ مِن قَبْلِكُمْ قَوْمِ نُوحٍ وَعَادٍ وَثَمُودَ ۗ وَالَّذِينَ مِن بَعْدِهِمْ ۗ لَا يَعْلَمُهُمْ إِلَّا اللَّهُ ۗ²

Bonyeza usikilize

- Mfano wa tatu:

Inapasa kusimamia neno **بَلَىٰ** au kusimamia neno **شَهِدْنَا** katika kauli ya Allaah:

وَإِذْ أَخَذَ رَبُّكَ مِن بَنِي آدَمَ مِن ظُهُورِهِمْ ذُرِّيَّتَهُمْ وَأَشْهَدَهُمْ عَلَىٰ أَنفُسِهِمْ أَلَسْتُ بِرَبِّكُمْ ۗ^ط
قَالُوا بَلَىٰ ۗ شَهِدْنَا أَن تَقُولُوا يَوْمَ الْقِيَامَةِ إِنَّا كُنَّا عَنْ هَذَا غَافِلِينَ ۗ³ ﴿١٧٢﴾

Bonyeza usikilize

² Ibraahiym (14: 9)

³ Al-A'raaf (7: 172)